JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SHINYANGA

# (SHUWASA)

# MKATABA WA KAZI YA UJENZI WA VITUO VYA KUCHOTEA MAJI, KUCHIMBA MITARO NA KULAZA BOMBA SHINYANGA MJINI KATIKA MRADI WA MAJI KWA FEDHA ZA UVIKO 19

MKATABA NAMBA: AE/046/2021-2022/W/11

KATI YA

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SHINYANGA (SHUWASA)

NA

MBARUKU RENATUS MYOVELA

S.L.P 10014 MWANZA

JANUARY, 2022



Scanned with CamScanner

## MKATABA

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 22 mwezi wa 02 ,2022.

**BAINA YA**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SHINYANGA (SHUWASA)** wa Sanduku la Posta 298 SHINYANGA (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "MWAJIRI") kwa upande mmoja

**NA**

**MBARUKU RENATUS MYOVELA** wa Sanduku la Posta 10014 MWANZA, (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "FUNDI UJENZI") kwa upande mwingine.

MWAJIRI na FUNDI UJENZI wote kwa pamoja watatambulika kama "WAHUSIKA"

**KWAMBA,** katika Mkataba huu MWAJIRI na FUNDI UJENZI inajumuisha warithi wao, wasimamizi wao, waangalizi wao na wale wote walio na haki dhidi yao kwa namna moja au nyingine.

**NA KWAMBA MWAJIRI** ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria katika kifungu namba 09 cha Sheria Ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namba 05 ya Mwaka 2019 na kupewa mamlaka ya kusambaza huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mkoa wa Shinyanga

**Kwamba FUNDI UJENZI** ni Fundi aliyejiajiri akifanya kazi za ufundi mbalimbali katika Mkoa wa Shinyanga MKATABA WA KAZI YA UJENZI WA VITUO VYA KUCHOTEA MAJI, KUCHIMBA MITARO NA KULAZA BOMBA SHINYANGA MJINI KATIKA MRADI WA MAJI KWA FEDHA ZA UVIKO 19

HIVYO BASI MWAJIRI anaingia MKATABA WA KAZI YA UJENZI WA VITUO VYA KUCHOTEA MAJI, KUCHIMBA MITARO NA KULAZA BOMBA SHINYANGA MJINI KATIKA MRADI WA MAJI KWA FEDHA ZA UVIKO 19 kwa kuzingatia vigezo na masharti kama ifuatavyo;

### 1.0 MALENGO YA MKATABA



Scanned with CamScanner

MWAJIRI kwa malipo maalumu kama ilivyoainishwa kwenye kipengele cha **2.0** cha Mkataba huu, anamuajiri FUNDI UJENZI kufanya ujenzi wa MKATABA WA KAZI YA UJENZI WA VITUO VYA KUCHOTEA MAJI, KUCHIMBA MITARO NA KULAZA BOMBA SHINYANGA MJINI KATIKA MRADI WA MAJI KWA FEDHA ZA UVIKO 19

## 2.0 GHARAMA

MWAJIRI atapaswa kumlipa FUNDI UJENZI kiasi cha shilingi za Kitanzania ***Milioni hamsini na sita laki nane elfu therasini tano Tu (Sh 56,835,000.00***) kwa mpangilio ulioyoainishwa katika kipengele 3.0 cha Mkataba huu.

## 3.0 TARATIBU ZA MALIPO

a)

| Item No. | Description of items | Quantity | Unit of measure | Unit Price | Total Price |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Excavation of trench, pipe laying, installation of fittings and backfilling width= 0.6m, depth= 1m | | | | |
| 1.1 | HDPE OD 110mm | M | 3500 | 3,900 | 13,650,000 |
| 1.2 | HDPE OD 90mm | M | 5000 | 3,900 | 19,500,000 |
| 1.3 | HDPE OD 75mm | M | 4100 | 3,900 | 15,990,000 |
| 1.4 | HDPE OD 32mm | M | 750 | 3,900 | 2,925,000 |
| 1.5 | Trench excavation (Hard soil formation); pipe laying and joining; installation of fittings; Trench backfilling width 0.6m, depth 1m | Cubic meter | 20 | 30,000 | 600,000 |
| | **Sub – Total 1:** | | | | **52,665,000** |
| 2.1 | Construction of water domestic points, consisting site clearance, setting out, excavation, concrete work, | NO | 4 | 300,000 | 1,200,000 |



Scanned with CamScanner

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | block work, plumbing work, finishing and curing during project implementation. | | | | |
| 2.2 | Construction of valve chambers, consisting site clearance, setting out, excavation, concrete work for foundation and slab, block work, plumbing work, finishing and curing during project implementation. | NO | 6 | 250,000 | 1,500,000 |
| 2.3 | Construction of marker posts, consisting formworks, steel fixing, concrete casting, labelling, placement on popeline and respective valves as instructed by engineer( 100m spacing) | NO | 140 | 10,500 | 1,470,000 |
| | **Sub – Total 2:** | | | | **4,170,000** |
| | **Total Costs for Shinyanga Municipal ( 1 &2 )** | | | | **56,835,000** |

b) Malipo yalioyoainishwa katika kipengele **3.0 (a)** cha Mkataba huu, yanapaswa kufanyika ndani ya siku thelathini (30) baada ya MWAJIRI kupokea hati ya madai (invoice) kutoka kwa FUNDI UJENZI.

## 4.0 **MUDA WA MAKUBALIANO**

Kwa WAHUSIKA kusaini Mkataba huu, makubaliano haya yatadumu kwa muda wa siku Mia na ishirini (120) kuanzia tarehe ya utekelezaji wa mkataba huu ambao ni mara baada ya kusainiwa kwa mkataba.



Scanned with CamScanner

## 5.0 MAJUKUMU YA MWAJIRI

Katika Mkataba huu MWAJIRI atakuwa na majukumu yafuatayo;

a) Kununua na kusafirisha vifaa kwa ajili ya ujenzi katika eneo la mradi.

b) MWAJIRI hatohusika na kulipa ada ya ongezeko la thamani VAT 18% au zaidi katika jumla ya gharama za ufundi walizokubaliana.

c) MWAJIRI atalipa gharama zote za ulinzi kwenye eneo la Mradi katika kipindi chote cha Mkataba huu.

## 6.0 MAJUKUMU YA FUNDI UJENZI

Katika Mkataba huu FUNDI UJENZI atakuwa na majukumu yafuatayo;

a) Kuhakikisha anatoa huduma zote za ujenzi zilivyo ainishwa katika Mkataba huu kwa mujibu wa maelekezo yatakayokuwa yanatolewa na MWAJIRI.

b) FUNDI UJENZI anatakiwa kufanya kazi yake ya ujenzi kwa umakini na uweledi na katika viwango kinacho zingatia maelekezo kutoka kwa MWAJIRI na endapo itabainika kuwa FUNDI UJENZI kafanyakazi chini ya kiwango atalazimika kurudia kazi hiyo kwa kufuata maelekezo ya MWAJIRI kwa gharama zake.

c) MWAJIRI ana haki ya kukagua kazi ya FUNDI UJENZI na ni jukumu la FUNDI UJENZI kutoa ushirikiano na msaada wowote pale utakapohitajika.

d) FUNDI UJENZI anatakiwa kuanza na kumaliza ujenzi katika kipindi walichokubaliana na MWAJIRI au kwa muda utakao ainishwa endapo Mkataba utauhuishwa.



Scanned with CamScanner

## 7.0 MABADILIKO KATIKA MKATABA

Maboresho, marekebisho na nyongeza yoyote katika mkataba huu yatatakiwa kuhuishwa kwa maridhiano ya maandishi kutoka pande zote mbili na kuambatanishwa katika mkataba huu.

## 8.0 UTATUZI WA MIGOGORO

WAHUSIKA wa Mkataba huu, watajitahidi kadri ya uwezo wao kutatua mgogoro wowote utakaojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu kwa njia ya maelewano.

## 9.0 KUVUNJIKA AU LISITISHWA KWA MAKUBALIANO

Pasipo kuathiri kipengele cha 7.0 hapo juu, upande mmoja unaweza kuvunja/kusitisha makubaliano haya wakati wowote iwapo upande huo utatoa notisi ya maandishi ya siku kumi na nne (14) kabla ya upande mwingine, wenye nia ya kuvunja/kusitisha makubaliano.

## 9.0 SHERIA TAWALA ZA MKATABA

Mkataba huu utaendeshwa kwa kuzingatia Sheria za Tanzania (Laws of Tanzania).

## 10.0 NOTISI

Notisi au taarifa iliyotajwa katika Mkataba huu inapaswa itolewe kwa njia ya maandishi na kutumwa kwa barau pepe au sanduku la posta g

**MWAJIRI:** - Barua pepe info@shuwasa.or.tz Sanduku La Posta 298 SHINYANGA;

**FUNDI UJENZI**: - Simu namba 0762557799 SHINYANGA.



Scanned with CamScanner

**KWA KUTHIBITISHA MKATABA HUU SISI WAHUSIKA** tunaweka saini zetu na kwa kushuhudiwa na mashahidi katika namna tarehe, mwezi na mwaka kama inavyoonyeshwa hapo juu.

**UPANDE WA MWAJIRI**

Jina Kamili: Eng. YUSUPH KATOPOLA

Wadhifa: KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI

Saini: ______________

Anuani: 298, SHINYANGA.

MANAGING DIRECTOR * SHINYANGA WATER SUPPLY & SANITATION AUTHORITY * SHUWASA

**SHAHIDI**

Jina Kamili: HAPPY RICHARD

Wadhifa: AFISA SHERIA

Saini: ______________

Anuani: 298 SHINYANGA

**UPANDE WA FUNDI UJENZI**

Jina Kamili: MBARUKU RENATUS MYOVELA

Wadhifa: FUNDI

Saini: ______________

Anuani: 10014, MWANZA

MBARUKU RENATUS MYOVELA LICENSED LOCAL FUNDI P.O. BOX 10014 MWANZA

**SHAHIDI**

Jina Kamili: AGNESS ALLY MYOVELA

Wadhifa: MKE

Saini: ______________

Anuani: 10014, MWANZA

Scanned with CamScanner